TANGAZO LA SERIKALI Na. 103 la tarehe 16/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWAKATIKA ENEO LA KAPULAMPUNGUTI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Kapulampunguti ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 59066MS, 8959053KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki mwa mto Ngubwisi katika uelekeo wa N90$^{0}$ 00' 00. MS kwa umbali wa kilomita 1.14 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 593208MS, 8959053KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS 71$^{0}$ 15' 50.49MS kwa umbali wa kilomita 0.61 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira-nukta 593790MS, 8958588KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki mwa ziwa Kingiri katika uelekeo wa KS 31$^{0}$ 27' 45.40 MS kwa umbali wa kilomita 0.31 hadi kwenye alama ya mpaka ya namba D yenye majira-nukta 593954MS, 8958588KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS 19$^{0}$ 54' 12.73MG kwa umbali wa kilometa 0.63 hadi kwenye alama ya mpaka namba E yenye majira-nukta 593741MS, 8957999KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea KaskaziniMagharibi katika uelekeo wa KZ 88$^{0}$ 41' 05.91MG kwa umbali wa kilomita 1.98 hadi kwenye alama ya mpaka namba F yenye majira-nukta 591763MS, 8958035KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 40$^{0}$ 41' 11.94MG kwa umbali wa kilomita 0.37 hadi kwenye alama ya mpaka wa namba G yenye majira-nukta 591522MS, 8958315KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 8$^{0}$ 27' 05.16 MG kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka namba H yenye majira-nukta 591504MS, 8958437KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea KaskaziniMashariki mwa shule ya msingi Ntaba katika uelekeo wa KZ 42$^{0}$ 24' 38.20MS kwa umbali wa kilomita 0.83 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 592066MS, 8959053 KZ unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*